**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**OFISI YA RAIS – KATIBA SHERIA UTUMISHI NA UTAWALA BORA**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA ZANZIBAR KWA MWAKA 2022/2023 KWA OFISI YA RAIS-KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

**SEPTEMBA 2023**

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana leo hii na kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2022/2023, yaliyotolewa na Kamati wakati wa kufuatilia utekelezaji wa Programu za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipatia fursa hii ya kuwasilisha Ripoti hii mbele ya Kamati yako. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na maelekezo yao yaliyotusaidia na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ni miongoni mwa Wizara zilizotembelewa na Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo pamoja na taasisi zake na kutoa maoni, maelekezo na ushauri uliosaidia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kipindi hicho cha 2022/2023 Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imetekeleza shughuli mbali mbali za kawaida na maendeleo pamoja na ahadi za Serikali zilizotolewa katika mkutano wa Bajeti wa mwaka 2022/2023 kwa kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati kupitia programu kuu 16 zinazotekelezwa na Idara na taasisi za Ofisi kama ifuatavyo: -

| PROGRAMU | IDARA/TAASISI |
|---|---|
| i. Programu ya Masuala ya Sheria; | Idara ya Msaada wa Kisheria; |
| ii. Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora; | Idara ya Utawala Bora; |
| iii. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini; | Ofisi ya Mufti Mkuu; na |
| iv. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa OR-KSUUB; | Idara ya Uendeshaji na Utumishi;<br>Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; na<br>Ofisi Kuu – Pemba; |

| | |
|---|---|
| v. Programu ya Uendelezaji wa Utumishi wa Umma; | Idara ya Mipango Raslimaliwatu; Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi; na Chuo Cha Utawala wa Umma (IPA). |
| vi. Programu ya Huduma za Serikali Mtandao; | Wakala wa Serikali Mtandao; |
| vii. Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa haki; | Mahkama; |
| viii. Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria; | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; |
| ix. Programu ya Usimamizi wa utekelezaji wa Kesi za Jinai; | Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka; |
| x. Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria; | Tume ya Kurekebisha Sheria; |
| xi. Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Raslimali za Umma; | Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; |
| xii. Programu ya Uzuiaji wa vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi; | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi; |
| xiii. Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma; | Kamisheni ya Utumishi wa Umma; na |
| xiv. Programu ya Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini. | Tume ya Utumishi Serikalini. |
| xv. Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi | Tume ya Maadili ya Viongozi; |
| xvi. Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana |

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika utekelezaji wa programu hizo Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepokea maoni na maagizo 66 kutoka Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2022/2023. Utekelezaji wa maagizo hayo ya Kamati ni kama inavyoonekana katika jeduweli lililoambatanishwa na taarifa hii.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Wajumbe wa Kamati wanaombwa waipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati pamoja na kushauri ipasavyo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** naomba kuwasilisha

**MWAL. HAROUN ALI SULEIMAN**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**

**ZANZIBAR**

| | IDARA/TAASISI HUSIKA | MAONI/USHAURI/MAAGIZO | MAJIBU |
|---|---|---|---|
| 1 - | Mahkama | Kamati inazishauri Mahkama ziendelee kufanya matengenezo ya majengo yake ya Mikoa ili kutanua wigo wa watendaji kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. | Katika kutekeleza ushauri wa Kamati, Mahkama ya Zanzibari imefanikiwa kuchukuwa hatua zifuatazo;<br>1. Kulifanyia ukarabati Jengo la Mahkama ya Mkoa wa Kaskazini lilioko Wete Pemba kwa hatua ya kuliezeka ili kulikinga na uharibifu unaosababishwa na kuvuja.<br>2. Kulifanyia ukarabati Jengo la Mahkama ya Mkoa wa Kusini lilioko Chake Chake Pemba, kwa hatua ya kuondosha mpira mchakavu katika "slab" na kuweka tarazo pamoja na kuweka miundombinu ya kushusha maji ya mvua.<br>3. Sambamba na hatua hizo za ukarabati, Mahkama ya Zanzibar iko katika hatua za mwisho za matayarisho ya ujenzi wa majengo ya Mahkama nyengine za Mikoa na Wilaya, Unguja na Pemba. |
| | | Kamati inatoa ushauri kwa wananchi kuzitumia Mahkama zilizo karibu nao badala ya watu wote kukimbilia Mahkama ya Mwanakwerekwe na hivyo | Mahkama ya Zanzibar imekuwa ikiendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kupunguza migogoro inayopelekea kufikishana Mahkamani.<br><br>Katika kulifanyia kazi tatizo la |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kuongeza msongomano wa watu; | msongamano wa watu Mahkama ya Mwanakwerekwe, tayari hatua zinaendelea kuchukuliwa kuengeza majengo ya Mahkama kwa kila Wilaya kwa lengo la kuipunguzia msongamano Mahkama ya Mwanakwerekwe. Kwa sasa Mahkama ya Mwanakwerekwe inatumikia Wilaya tatu, ikiwemo Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi A na Wilaya ya Magharibi B. |
| | | Kamati inaishauri Mahakama kuweka utaratibu maalum wa kupeleka gari ya Mheshimiwa Jaji Mkuu Kisiwani Pemba. | Mahkama ya Zanzibar tayari imeshafanya maombi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kwa ajili ya gari ya Mheshimiwa Jaji Mkuu kisiwani Pemba. |
| | | Kamati inaishauri Serikali kuzisaidia Mahkama hususan Mahkama ya Kadhi kupatiwa vyombo vya usafiri ili kuwasaidia katika kutekeleza shuhguli zao. | Gari mpya kwa ajili ya matuimizi ya Kadhi Mkuu imepatikana. Gari mbili za Naibu Kadhi Mkuu na Mrajisi wa Mahkama ya Kadhi zipo licha ya kuwa na umri mkubwa na kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara.<br><br>Ukosefu wa Gari unaoendelea ni kwa ajili ya Kadhi wa Rufaa Pemba na Gari kwa kazi za ufuatiliaji Unguja na Pemba.<br>Mahkama ya Zanzibar ilishawasilisha Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, mahitaji ya gari kwa ajili ya Kadhi wa rufaa wa Mahkama ya Kadhi Pemba. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Kamati inashauri Mahkama ya Kadhi nayo kupatiwa ulinzi wa kutosha wakati wa uendeshaji wa kesi kwani kufanya hivyo kutawajengea imani Mahakimu wetu wakati wa kutoa hukumu za kesi katika Mahkama hizi. | Hatua za kuonana na Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar zimefanyika kwa ajili ya kuipatia Mahkama ya Kadhi askari.<br>Hata hivyo, utekelezaji wake haujakamilika kutokana na changamoto ya uhaba wa askari katika Jeshi la Polisi.<br>Kwa sasa Mahkama ya Kadhi ina Askari Polisi mmoja tu, hapo Mwanakwerekwe. |
| | | Kamati inaishauri Mahkama kuifanyia matengenezo nyumba ya Mheshimiwa Jaji Mkaazi Kisiwani Pemba pamoja na kupatiwa samani (furniture) mpya na zenye uhakika wa matumizi. | Ukarabati na upatikanaji wa samani mpya katika nyumba ya Jaji Mkaazi Pemba unatarajiwa kufanyika katika robo ya pili ya mwaka wa Fedha 2023/2024. |
| 2 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | Kamati inashauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuliangalia suala la usafiri kwa upande wa Pemba ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. | Ofisi imepanga ununuzi wa magari mawili (2) katika Mpango kazi wa 2022/23 kwa upande wa Unguja na Pemba na utekelezaji wake wa upatikanaji wa magari hayo upo katika utaratibu wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. |
| | | Kamati inaziomba Taasisi ambazo zinalalamikiwa kuharakisha majibu ya walalamikaji ili kuwarahisishia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kumaliza | Ofisi inasimamia ushauri huo kwa kufuatilia taasisi hizo zinazolalamikiwa kuharakisha majibu ya walalamikaji ili kuwarahisishia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kumaliza mashauri yao kwa wakati. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | mashauri yao kwa wakati. | |
| 3 | Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) | Kamati inaishauri Ofisi ya DPP kuongeza bidii ya kuwasomesha watendaji wake kwa lengo la kupata wataalamu zaidi wa kusimamia na kuendesha kesi. | Ofisi imewapatia nafasi za masomo watendaji wake ili kuwaongezea uwezo wa kitaaluma na waweze kufanya kazi zao kwa uweledi ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya wafanyakazi wawili (2) wamepatiwa Mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya Pili ya Sheria na kwa upande wa Mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi kumi (10) wamepatiwa mafunzo elekezi ya sheria ya uendeshaji wa kesi za jinai, na wafanyakazi (16) wamepatiwa mafunzo katika kada za utawala. |
| | | Ofisi ifanye Mpango wa kukitangaza Kituo cha Utafiti wa Sheria Zanzibar ili kuongeza wanafunzi kutoka sehemu mbali mbali nje ya Zanzibar. | Kituo kinajitangaza kupitia vyombo mbali mbali vya Habari hasa Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) |
| | | Kamati inaishauri Ofisi kutumia mbinu mbadala ya kuwatumia Masheha na viongozi wa Dini kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kufika Mahkamani na kutoa | Ofisi inashirikiana na Masheha na Taasisi nyengine za haki jinai katika kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutoa ushahidi Mahakamani kupitia programu za elimu kwa jamii (outreach Programme). Ambapo kwa mwaka wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | ushahidi. | fedha 2022/2023 Shehia za Nungwi Banda Kuu na Fuoni Skuli kwa Unguja na Shehia za Micheweni Maziwa Ngombe na Vitongoji kwa Pemba zimefikiwa katika kupatiwa elimu hiyo. Aidha Afisi inategemea kuendelea na programu hizo katika mwaka huu wa fedha ili kukuza uelewa kwa wananchi na kupunguza tatizo la wananchi kutofika mahakamani kutoa ushahidi. |
| | | Kamati pia inaishauri Ofisi kufuatilia kwa ukaribu changamoto ya usafiri na kulipatia ufumbuzi kwa kadri hali inavyoruhusu. | Ofisi imepata ahadi kutoka Serikalini ya kupatiwa magari mawili (2) kwa ajili ya kurahisisha shughuli za Uendeshaji wa Mashtaka.<br>Aidha, katika bajeti ya mwaka 2023/2024 Ofisi imepanga kununua gari kwa upande wa Unguja na Pemba. |
| | | Kamati inaiomba Serikali kuangalia kwa umuhimu wake suala la wananchi kubambikiziana kesi za udhalilishaji bila ya kuwepo ukweli wake au kwa lengo tu la kuchafuana. | Serikali kupitia taasisi zake za kusimamia Haki Jinai na taasisi nyengine zimekuwa na programu mbali mbali za kuelimisha jamii juu ya athari ya kutoa ushahidi wa uongo kwa kosa ambalo mwananchi hajalifanya. Hatua za kisheria huchukuliwa pindi ikibainika kuwa kesi hiyo ya kubambikizana na haina ukweli wowote. |
| | | Kamati inashauri ofisi hii kuwachukulia hatua wale wote wenye kupeleka kesi za udhalilishaji kwa kupanga au | Ofisi inahakikisha majalada yote yanayoingia yanapatiwa kwa umakini ili kuondosha uwezekano wa kushtakiwa mtu kwa uonevu. Aidha, Ofisi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kukusudia kuchafuana katika jamii. | inazingatia vyema ushauri huu wa Kamati. |
| 4 | Tume ya Kurekebisha Sheria | Kamati inaishauri Serikali kuipatia Tume jengo la kisasa ambalo litakidhi haja kwa wafanyakazi wake. | Jitihada mbalimbali zimechukuliwa ikiwemo kuandika barua ya kuomba eneo katika Mamlaka ya Ardhi, kukutana na Waziri wa Ardhi pamoja na Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Ardhi. Aidha, vikao vya mara kwa mara vimefanyika kwa watendaji na hatua iliyofikiwa na Wizara imetuahidi hivi karibuni kupatiwa kiwanja katika eneo la Kwanyanya. Hivyo, kwasasa tunasubiri majibu kutoka Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kuendelea hatua nyengine za ujenzi wa jengo la Kisasa ambalo litakidhi haja kwa wafanyakazi wake. |
| | | Kamati inashauri Tume kuzifanyia mapitio sheria zote zenye kuleta ugumu wa utekelezaji wake kila inapoona inafaa kufanya hivyo. | Tume inaendelea kufuata ushauri kwa kuzifanyia mapitio Sheria mbalimbali zikiwemo Sheria za zamani sana ambazo haziwezi kuendelea kutumika kwa sasa kutokana na kupitwa na wakati. Jumla ya Sheria tisa (9) zimepitwa na wakati nazo ni:- Sheria ya Ukomo ya muda sura ya 12 mwaka 1917, Sheria ya Uhaulisho ya mwaka 1917, Sheria Ya Ufilisi ya mwaka 1917,Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam.7 ya 1997, Sheria ya kukinga na kusimamia masuala ya Ukimwi nam 18 ya 2013, viapo vya Utii na barua za |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | uteuzi nam 1 ya 1986, Sheria ya Mirathi (watu wasiokuwa waiislam) sura ya 21 mwaka 1917, Viapo sura ya 7 ya 1917 na Sheria ya kulinda utamaduni wa Taifa nam 1 ya 1917. |
| | | Kamati inazishauri taasisi za Serikali kutoa mashirikiano ya moja kwa moja na Tume ili kuzipitia sheria za taasisi zao kwa ufanisi zaidi. | Tume imendelea kupata mashirikiano kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali na kuweza kufanya mapitio ya baadhi ya Sheria. Miongoni mwa Sheria ambazo zimefanyiwa Mapitio kwa kushirikiana na taasisi nyengine ni Sheria ya mtoto, Sheria ya Takwimu na nyenginezo. |
| | | Kamati inaishauri Serikali kuunga mkono juhudi za Tume kwa kuwapatia fedha za kutosha za matumizi kwa wakati ili kusaidia kutoa mafunzo kwa watendaji wake na kutoa elimu kwa jamii. | Serikali inaendelea kufanya Jitihada za kuunga mkono juhudi za Tume kwa kuipatia Fedha za matumizi kwa wakati kadri hali ya fedha inavyokuwa lengo ni kusaidia kutoa mafunzo kwa watendaji wa Tume kwa ajilii ya kutoa Elimu kwa jamii. |
| | | Kamati inaishauri Serikali kufanya utaratibu wa kuongeza wataalamu wa sheria kwa kuajiri au kuhamisha kutoka ofisi moja na kwenda Tume ili kuongeza nguvu katika utekelezaji wa majukumu yao. | Serikali inaendelea kufanya jitihada ya kuengeza wataalamu wa Sheria kwa kuajiri na kuhamisha wanasheria hao kutoka Ofisi moja kwenda Tume kwaajili ya kuongeza nguvu katika utekelezaji wa majukumu yao na kwasasa tayari ruhusa ya kuajiri wanasheria wanne (4) kwa mwaka 2023/2024. |
| 5 | Skuli ya Sheria Zanzibar | Kamati inaishauri Serikali kuipatia Skuli majengo yake | Hatua za kupata Kiwanja cha ujenzi wa Jengo la Skuli ya Sheria zimekamilika. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | ya kudumu ambayo yatasaidia kufikia malengo ya Skuli licha ya harakati hizi kuanza lakini bado juhudi za makusudi zinahitajika ili kufikia malengo kwa wakati. | Uongozi wa Skuli ya Sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora umeshafanya mazungumzo na wadau wa maendeleo ikiwemo Benki ya Dunia (World Bank) kuangalia uwezekano wa kupatiwa msaada wa ujenzi wa jengo hilo. |
| | | Skuli ifanye jitihada ya kuweka maktaba yenye vitabu vya kutosha kwa ajili ya wanafunzi ili kuwarahisisshia katika masomo yao. | Hatua za awali za kuwa na Maktaba zimeshaanza kwa kutafuta vitabu vichache sana vilivyopo Ofisi ya Skuli ya Sheria katika Jengo la Kamisheni ya Utumishi wa Umma Mwanakwerekwe. Hata hivyo, Uongozi wa Skuli umekuwa ukichukuwa jitihada za kuzungumza na wafadhili kwa ajili ya kuimarisha Maktaba hiyo. |
| | | Skuli ifuatilie kikamilifu suala la usafiri na kutatua changamoto hii kwa wakati. | Skuli ya Sheria tayari imepatiwa gari moja aina ya "Pick up" kwa ajili ya matumizi ya Ofisi. Hata hivyo, Skuli ya Sheria imeahidiwa kupatiwa gari ya pili na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango hivi karibuni. |
| | | Skuli ijitangaze zaidi katika maeneo mengi ya nchi na maeneo ya nchi jirani ili kuongeza idadi ya wanafunzi na kupata mapato zaidi. | Hatua za kuitangaza Skuli zimeanza kwa kuanzisha vipindi vya Radio na Televisheni. Pia Skuli imedhamiria kutoa matangazo ya udahili ndani na nje ya nchi kwa kutumia vyombo vya habari mbali mbali. |
| 6 | Kamisheni ya Wakfu na | Kamisheni izidishe bidii | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mali ya Amana | katika kutoa elimu ya mirathi kwa jamii. | inaendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia ZBC Redio kwa kila Ijumaa saa 1:30 usiku kuhusu masuala mbali mbali ya dini ya kiislamu ikiwemo suala la mirathi kupitia utaratibu wa kiislamu. Kamisheni imeweka Afisa wake katika Wilaya zote za Unguja na Pemba ambapo mikutano ya uelimishaji hufanyika kwa kujumuisha masheha, vikundi maalum na wananchi kwa ujumla. Kamisheni imeanzisha Jarida la kieletroniki linalotoka kila baada ya wiki mbili na kutumia Tovuti na mitandao ya kijamii ikiwemo Facebook na Instagram ili kuelimisha jamii juu ya majukumu yake ikiwemo usimamizi na uendeshaji wa mirathi. |
| | | Kamati inaishauri Kamisheni kusimamia ipasavyo na kuweka taarifa sahihi za mashamba ya Wakfu kwa Unguja na Pemba sambamba na kuzitambua mali zote za Wakfu ambazo kwa muda mrefu hazitumiki kisheria. | Kamisheni imeanzisha "Database" ya Kieletroniki ya usimamizi wa Mali za Wakfu na Amana na majaribio yameanza kwa kuingizwa taarifa za mali hizo. Mpango wa kuyaendeleza mashamba na mali nyengine umeshaandaliwa ili kutoa tija zaidi kwa wanufaika wake. |
| | | Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Mwanansheria Mkuu kuwatambua wanasheria wa Kamisheni kama Mawakili wa | Tayari Kamisheni ina Wakili mmoja wa Serikali "State Attorney" aliepatikana kwa njia ya uhamisho na imefanya mazungumzo na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuongezwa mawakili wawili. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Serikali ili kwenda sambamba na taasisi nyengine za umma ambazo zimekuwa na wanasheria wa kuzisaidia taasisi zao kusimamia haki na fursa zao. Aidha, Kamisheni inapaswa kufuatilia kwa ukaribu suala hili ambalo zaidi limeathiri ofisi ya Pemba kiutendaji. | |
| | | Kamati inahimiza kuajiri vijana wa kutosha wakiwemo wataalamu wa mirathi ili kuwawezesha kutoka hatua waliyosasa na kwenda hatua nyengine ya kiuzalishaji baada ya kupata wataalamu wa kiuchumi kutoka Serikalini. | Kupitia Mpango wa Uajiri wa Mwaka 2023/24 Kamisheni imedhamiria kujaza nafasi tupu 22 kwa kuajiri wataalamu wa fani mbali mbali wakiwemo wa Mirathi na Zakka ili kutoa huduma bora kwa wananchi na kuiwezesha Kamisheni kujiendesha kisasa na kutoa tija kwa Taifa. |
| | | Kamati inapendekeza kwa Serikali kuiangalia Kamisheni ya Wakfu kwa njia iliyo bora ya utaratibu wa malipo ambao hautosumbua shughuli za utekelezaji wa Ofisi hiyo. | Kamisheni imeshaomba muongozo Wizara ya Fedha ili kuwa na utaratibu wa malipo wenye ufanisi zaidi katika kutoa huduma kwa wananchi. |
| | | Kamati inaiomba Kamisheni kuharakisha marekebisho ya Sheria ili iweze kukidhi haja ya masuala yote ya mirathi na mambo mengine. | Mswaada wa Sheria mpya umeshaandaliwa na upo katika hatua za mapitio ili kuwasilishwa katika Mamlaka husika kwa mapitio zaidi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7 | Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar | Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar isichoke kuchukua hatua na kutoa miongozo ya kidini wakati wote wanapoona inafaa. | Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar inaendelea kuchukua hatua na kutoa miongozo ya kidini kila inapohitajika kufanya hivyo. |
| | | Kamati inashauri kuharakisha suala la migogoro mbali mbali ambayo inaletwa kwao ili iweze kumalizika kwa muda mfupi. | Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar inaendelea na utaratibu wa utatuzi wa migogoro kwa haraka iwezekanavyo. Hata hivyo, ipo migogoro inayomaliza ndani ya kikao kimoja na baadhi ya migogoro huchukua vikao viwili visivyopindukia wiki mbili. |
| | | Kamati inaelekeza Ofisi ya Mufti kuongeza vipindi vya kuelimisha jamii juu ya masuala mbali mbali ya dini na kupitia hutba za sala za ijumaa wanazoziandaa. | Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar imepokea maagizo hayo na inaendelea kuongeza vipindi vya kuelimisha jamii juu ya masuala mbali mbali ya dini na kutoa miongozo kwa makhatibu wa Ijumaa kila yanapotokezea matukio muhimu katika jamii (burning issues). |
| 8 | Tume ya Utumishi Serikalini | Kamati inashauri Tume kutoa elimu ya uelewa wa Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni zake kwa watumishi wote wa sekta za umma. | Elimu ya uwelewa wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma imeendelea kutolewa katika ngazi zote za watumishi kwa kushirikiana na taasisi za umma husika. |
| | | Kamati inashauri Tume kutoa uwelewa kwa watumishi juu ya mikataba ya kazi pamoja na mambo yote muhimu yanayohusiana na Utumishi kama vile ardhilhali na barua | Jukumu hili linatekelezwa kupitia Wizara na Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambapo Tume ya Utumishi imejipanga kulitekeleza katika bajeti ijayo ya mwaka wa fedha 2023/2024. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | ya kuthibitishwa kazi. | |
| | | Tume inashauriwa kuwachukulia hatua watumishi wenye kutekeleza majukumu yao kinyume na Sheria na Kanuni za utumishi wa umma. | Tume kwa kawaida imekua ikiwachukulia hatua za kinidhamu watumishi kwa mujibu wa Sheria No 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 wanapobainika wamefanya kosa. |
| | | Kamati inashauri Tume kuweka utaratibu wa kuzikagua Taasisi za Umma ili kubaini mapungufu yanayojitokeza. | Utaratibu wa kuzikagua Taasisi za Umma upo kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa mujibu wa kifungu cha 25(i) cha Sheria ya Utumishi wa Umma. |
| | | Kamati inaishauri Tume kuweka uwazi katika mfumo wa ajira ili wananchi wafahamu kila hatua inayopitiwa katika utoaji wa nafasi mpya baada ya kutangazwa. | Tume inaendelea kuweka wazi mchakato wote wa uajiri kwa sababu hatua zote zinatangazwa katika vyombo vya habari na tovuti zake husika lakini pia Tume imeweka namba za simu na Baruapepe (email) kwa ajili ya kuwasaidia waombaji pindi wanapokwama kufanya maombi. Vile vile Tume inajipanga kutoa mafunzo katika maonesho pindi mfumo utakapomalizika. |
| 9 | Chuo cha Utawala wa Umma(IPA) | Kamati ilipata kutembelea na kukagua eneo la Mfikiwa lenye kiwanja cha Chuo kwa upande wa Pemba na kuona changamoto zilizomo katika eneo hili. Kamati haikuridhishwa na eneo hili kwa ujenzi wa Chuo na hivyo, | Chuo kwa kushirikiana na Afisa Mdhamini wa OR-KSUUB kimechukua jitihada za kufanya mazungumzo na Afisa Mdhamini wa Wizara ya Kilimo na kujadiliana kuhusu eneo la kiwanja lililopo Pujini Pemba na Chuo kimeagizwa kupeleka Mpango wa Ujenzi *“Site Plan”* hivyo Chuo kinasubiri |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuzuia ujenzi ambao umepangwa kufanywa katika eneo hili na hivyo kutafuta eneo jengine ambalo litakuwa rafiki katika mazingira ya Chuo lakini pia halitaigharimu Serikali fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi. | majibu kutoka Wizara ya Kilimo ili kianze mchakato wa ujenzi. |
| | | Ili Chuo kuweza kukusanya mapato na kujiendesha kama taasisi ya elimu, Kamati inashauri wanafunzi ambao hawalipi ada ya masomo kuzuiliwa matokeo yao ya mitihani au kuzuiliwa vyeti vyao vya masomo mpaka watakapokamilisha malipo ya ada. | Chuo kinaendelea kuchukua jitihada mbalimbali za kuweza kuongeza mapato, hivyo Chuo kinaendelea kuzuia matokeo na vyeti vya kumalizia masomo kwa wanafunzi wanaodaiwa sambamba na kuandaliwa kwa Kanuni na Miongozo ya Chuo kwa Wanafunzi itayoelezea bayana juu ya taratibu za malipo kabla ya kuendelea na masomo yao, pamoja na hatua itakayochukuliwa endapo Wanafunzi hawatofuata taratibu za malipo kama itakavyo elekezwa. |
| | | Kamati inashauri Chuo kutoa elimu na matangazo zaidi kwa taasisi za Umma juu ya umuhimu wa kupatiwa mafunzo elekezi pamoja na mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi. | Chuo kipo kwenye hatua za mwisho za maandalizi ya ratiba ya mwaka ya kutoa mafunzo kwa Viongozi na watumishi wa Umma, hatua itayofuata ni kuiwasilisha ratiba Wizarani kwa ajili ya kutolewa taarifa juu ya ushiriki wa mafunzo pamoja na kutoa matangazo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | katika vyombo vya habari, tovuti na mitandao ya kijamii. |
| | | Chuo kizidishe kasi ya kutafuta wafadhili kwa ajili ya kujenga jengo la utawala ili kukidhi mahitaji ya Chuo katika ngazi za utawala. | Chuo kinaendelea kutafuta wahisani wa kusaidia kuondoa changamoto hiyo. Ujenzi wa Jengo la Utawala (Administration Block). Kwa sasa Chuo kimefanya mazungumzo na Benki ya Kiisalamu (PBZ) na pia mazungumzo yanaendelea na TEA juu ya ujenzi wa Jengo. |
| | | Kamati haikuridhishwa na maendeleo ya Chuo kwa upande wa Pemba na hivyo, tunashauri Serikali iwekeze zaidi katika kusimamia na kuimarisha maendeleo ya Chuo hiki kwa Pemba. | Chuo kinafanya jitihada za ziada katika kukiimarisha kwa upande wa Pemba, ikiwemo ujenzi wa Jengo la Tawi la Chuo cha Utawala wa Umma pamoja na kushirikishwa kwa kila kinachofanyika Unguja na Pemba kinafanyika kwa ufanisi. |
| 10 | Kamisheni ya Utumishi wa Umma | Maslahi ya watendaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma yaboreshwe ili kwenda sambamba na majukumu wanayoyatekeleza. | Maslahi ya Viongozi na watendaji yameboreshwa. |
| | | Katika kujenga Utumishi ulio bora na wenye tija kwa wananchi, watendaji wa Serikali na Mashirika yasio ya Kiserikali ni lazima yakubaliane na miundo ya kiutumishi iliyopo ili kutoa | Kamisheni inaendelea kuzisimamia taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma, Wakala Tendaji na Kampuni kutekeleza Miundo ya Utumishi iliyoidhinishwa na Serikali ili kutoa huduma bora kwa wananchi. Mashirika yasio ya kiserikali hayahusiki katika Muundo wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | huduma bora kwa wananchi | Utumishi |
| | | Kamati inaishauri Kamisheni kuzifuatilia kwa kina Tume za Utumishi ili kuhakikisha zinatenda haki na zinawasimamia watumishi katika kutimiza wajibu wao kwa jamii. | Kamisheni inazifuatilia kwa kina Tume za Utumishi kwa kufanya Kaguzi, kufanya vikao maalumu na watendaji wa Tume hizo wakiwemo makatibu kwa kila robo mwaka na kuzisisitiza Tume kuhakikisha zinatenda haki katika kutekeleza majukumu yake. |
| | | Kamisheni ihakikishe inaidhinisha miundo ya taasisi ambazo zina sababu za msingi kufanya mabadiliko na sio kufanya mabadiliko kwa kufuata utashi wa wakuu wa taasisi au kuangalia upande mmoja wa maslahi ya taasisi husika. | Ushauri umepokelewa. Aidha, Kamisheni katika kuidhinisha Miundo inazingatia kifungu cha 50(2) cha Sheria ya Utumishi wa Umma No 2 ya 2011. |
| | | Kamati inaiagiza Kamisheni kufuatilia kikamilifu Taasisi zote ambazo zimeshaidhinishiwa miundo mipya na kuona utekelezaji wake. Hata hivyo, ni vyema ukawepo mpango maalumu wa ukaguzi kwa kila mwaka | Kamisheni inaendelea kufanya kaguzi juu ya Utekelezaji wa Miundo ikiwemo Miundo ya Utumishi kwa Wizara 18 za SMZ Unguja na Pemba na Ukaguzi huo utaendelea kwa Miundo ya Taasisi kwa mwaka wa Fedha 2023/2024. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kwa taasisi zote za umma. | |
| 11 | Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) | Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuboresha maslahi ya Ofisi ya CAG na hivyo kwenda sambamba na wakaguzi wengine wenzao wa Tanzania Bara. | Pongezi zimepokelewa, aidha Serikali inaendelea na jitihada zake za kuboresha maslahi ya watumishi wote wa umma Zanzibar kila hali itaporuhusu. |
| | | Kwa kuwa taasisi hii inajukumu la msingi katika kukagua na kudhibiti hesabu za Serikali, Kamati imeona ipo haja sasa kwa Serikali kumuwezesha CAG kufanya ukaguzi wa miundombinu, ukaguzi wa majengo ya Umma na ukaguzi wa vifaa vya kazi | Serikali imetoa kibali cha kuajiri watumishi wapya nane (8) kwa mwaka wa fedha 2023/2024 katika kada ya wakandarasi na mfamasia ili kukabiliana na changamoto hii. |
| | | Serikali kuangalia kwa kina umuhimu wa fedha za matumizi mengineyo kwa taasisi hii, kwani kiwango wanachopata hakilingani na | Ofisi imechukua hatua ya kuiandikia Serikali juu ya changamoto ya upungufu wa fedha za matumizi mengineyo na kuahidiwa kupatiwa kiwango cha fedha kwa mujibu wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | majukumu yao. | bajeti kila hali itaporuhusu ili kufanikisha mipango mizuri iliyojipangia. |
| | | Serikali iweke mkakati maalumu wa kuipatia taasisi usafiri wa uhakika. Kamati inashauri CAG ni vyema akapewa uwezo wa kununua gari zake mwenyewe badala ya kusubiri mgao kutoka Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango. | Ofisi imechukua jitihada za kuomba usafiri wa uhakika Serikalini na kufanikiwa kupata toyota Rava4 moja. Aidha, Ofisi ina matarajio ya kupata gari zaidi kutoka Serikalini ili kurahisisha utendaji kazi kila hali itaporuhusu. |
| | | Kamati pia, inaishauri Serikali kuiwezesha Ofisi kujiendesha kitaalamu kwa kupatiwa nyenzo na wataalamu watakao isaidia Serikali kuokoa fedha nyingi kupitia miradi ya maendeleo. | Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendelea kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na vitendea kazi pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wa Ofisi ya Mdhibiti ndani na nje ya nchi. Aidha, Ofisi imepatiwa nafasi mpya za kuajiri wataalamu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 ikijumuisha wataalamu wa Kodi, Bima na Vihatarishi, Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA, mfamasia, wakandarasi nk.<br>Vile vile kupitia M.O.U ilipo baina ya taasisi mbili za ukaguzi za Tanzania imeiwezesha Ofisi kushirikiana katika ukaguzi na kubadilishana wataalamu jambo ambalo linapelekea serikali kusimamia fedha zinazoelekezwa katika miradi ya maendeleo. |
| 12 | Wakala wa Serikali Mtandao (EGAz) | Ili kufikia lengo na dhamira ya kuanzishwa kwa Wakala | Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar inahakikisha kuwa malengo ya Serikali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | wa Serikali Mtandao Zanzibar, Kamati inaishauri Serikali kusimamia kikamilifu maendeleo ya Wakala ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. | ya kutoa huduma Bora kwa Wananchi yanafikiwa kwa kuzingatia matumizi ya mifumo ya TEHAMA kama ilivyobainishwa katika ilani ya Uchaguzi ya CCM. |
| | | Kamati imebaini kuwa mifumo ya Serikali Mtandao inayotumika na Taasisi za Umma haina ubora na imekuwa ikileta ugumu wa kutoa huduma kwa wananchi. Hivyo, Kamati inashauri kabla ya kuanza kutumika kwa mifumo hiyo Wakala ianze kufanya majaribio na kukusanya maoni ya wananchi juu ya matumizi bora ya mifumo hiyo. | Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar inafanyakazi kwa kushirikiana na wateja wake (Taasisi za Umma) katika kuandaa mifumo shirikishi ambayo hutumika katika Taasisi zote za Umma. Aidha, Wakala imekuwa inasimamia na kutoa mapendekezo kwa mifumo inayotaka kutengenezwa na Taasisi moja moja kwa matumizi ya Taasisi hizo za Umma.<br><br>Sambamba na hayo, Wakala inapopokea maombi ya kuanzisha mfumo kutoka kwa taasisi za Umma inakaa pamoja na taasisi husika kwa kushauriana namna bora ya mfumo unavyoweza kufanya kazi nakuleta tija kabla ya kusanifu mfumo huo. |
| | | Kamati inashauri Wakala kutafuta na kupendekeza kuajiriwa wataalamu wenye uzoefu katika fani za IT ili kusaidia maendeleo ya | Ushauri umepokelewa.<br><br>Aidha, Wakala imekua ikiomba maafisa TEHAMA wazoefu kutoka katika Taasisi za Umma kwa lengo la kuimarisha |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | teknolojia ya habari nchini. | nguvu kazi ya Wakala na kuongeza kasi ya utayarishaji na usimamizi wa Mifumo ya Kidigitali ambayo itarahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma za Serikali. |
| | | Wakala isimamie na ihakikishe Taasisi zote za Serikali zimefikiwa na mifumo stahiki ya mtandao ili kuweka uwiano wa kutoa huduma baina yao. | Wakala wa Serikali Mtandao inahakikisha kwamba Taasisi zinafikiwa na zinatumia miundombinu na mifumo shirikishi inayoanzishwa ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Serikali na utoaji wa huduma kwa Wananchi. |
| | | Wakala ichukue hatua kwa Taasisi zote za Umma ambazo zitaenda kinyume na miongozo ya matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika kutoa huduma kwa umma. | Ushauri umepokelewa.<br>Aidha, Wakala inachukuwa hatua kwa taasisi yoyote ambayo haifuati miongozo ya uanzishaji na matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa umma pamoja na ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA ambavyo havina sifa na viwango vilivyowekwa na Wakala. |
| 13 | ZAECA | Kamati inaishauri ZAECA kuzidi kuwaimarisha watendaji wake kwa kuwapatia elimu na mafunzo ya kutosha ya kukabiliana na uhalifu wa kuhujumu uchumi. | Mamlaka inaendelea na utaratibu wa kuwapatia mafunzo gani na watumishi wangapi mbalimbali watumishi wake ili kuweza kukabiliana na uhalifu wa kuhujumu uchumi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Ofisi ya ZAECA kushirikiana kikamilifu na Taasisi ya Ubora wa Viwango Zanzibar – ZBS katika kudhibiti matumizi ya bidhaa zilizopitwa na wakati (expire date) hususan bidhaa za vyakula na vipodozi. | Mamlaka imekuwa ikishirikiana na ZBS katika udhibiti wa bidhaa zilizopitwa na wakati (vyakula dawa na vipodozi) ambapo baadhi ya wafanyabishara waliobainika kuwa na bidhaa zilizopitwa na wakati wamekuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria. Pia inashirikiana na ZBS katika kudhibiti mapato yatokanayo na uingizwaji wa bidhaa mbali mbali nchini. |
| | | Kamati inaishauri Serikali kusaidia upatikanaji wa vyombo vya usafiri kwa ZAECA ili kuboresha utekelezaji wa majukumu yao. | Kwa kulifanyia kazi suala hili Mamlaka imeshakamilisha na kuwasilisha Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango barua ya maombi ya magari ili kuweza kurahisisha utendaji kazi wa Mamlaka. |
| | | Kamati inaishauri ZAECA kusimamia upatikanaji wa vitendea kazi vya kisasa kwa kusihirikiana na Serikali juu ya umuhimu wa vifaa hivyo katika kuimarisha maendeleo ya uchumi nchini. | Mamlaka imeshaiandikia serikali kuiomba upatikanaji wa vifaa vya kisasa na vya kitaalamu vya kufanyia uchunguzi ili kuweza kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka katika kazi zake za kila siku. |
| | | Kamati inaishauri ZAECA kuhakikisha wamejipanga katika kudhibiti hatua za awali za kutenda rushwa na uhujumu wa uchumi katika Taasisi za Umma na Binafsi ili kuepuka kutumia nguvu kubwa kutokana na matendo | Mamlaka inaendelea na hatua mbalimbali za kudhibiti vitendo vya rushwa na Uhujumu Uchumi ikiwa ni kipaombele kwa sasa. Hatua hizo zinajumuisha ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za matumizi ya kawaida (OC), ufuatiliaji wa miradi mbali mbali inayotekelezwa na Serikali pamoja na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | hayo | ufuatiliaji katika ofisi za umma zenye kukusanya mapato. |
| | | Serikali inashauriwa kwamba, ni vyema kwa ZAECA kupatiwa asilimia ishirini na tano (25%) ya fedha wanazookoa kutokana na rushwa na uhujumu uchumi ili iwe ni njia moja wapo ya mapato kwa taasisi hii. | Ushauri umepokelewa na tutaufanyia kazi. |
| 14 | Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma | Kamati inaishauri Wizara kuendelea na hatua za kuongeza watumishi wenye sifa zinazohitajika kulingana na Taasisi za Serikali. | Tume imepata mfanyakazi mmoja kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Kadhalika, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa ushirikiano na Tume ya Utumishi Serikalini imekamilisha utaratibu wa nafasi mbili (2) za ajira mpya na kupata watumishi wawili (2) wapya wa kada ya Sheria, ambao tayari wameanza kazi. |
| | | Kamati inashauri kuwatafutia Ofisi Tume ya Maadili kisiwani Pemba ambayo itaendana na hadhi ya Ofisi hiyo na kufanya kazi bila ya matatizo yoyote. | Ushauri umepokelewa na kufanyiwa kazi, lakini kutokana na ugumu wa kupata Ofisi Pemba, Tume inaendelea kufanya ukarabati wa jengo la Ofisi yake liliopo Chake Chake Pemba ili liendane na hadhi ya Ofisi. |
| | | Kamati inaishauri Tume ya Maadili kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake namna bora ya kuweza kudhibiti siri zinazotokana na ujazaji fomu. | Tume imefanikiwa kuendesha mafunzo maalum ya ndani (in house training) kwa watumishi wake yanayohusiana na matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Viongozi wa Umma pamoja na utunzaji wa siri za |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | taarifa za viongozi. |